

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA

06 MEI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA – TAREHE 06 MEI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2018/2019.

III. MASWALI:



OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**166. MHESHIMIWA RUTH HIYOB MOLLEL (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mtambo wa kuchoma takataka za Hospitali na Dawa zilizokwisha muda wake upo katika Kijiji cha Dandani Wilayani Mkuranga. Uchomaji unapofanyika

moshi mzito huingia kwenye nyumba na maeneo ya Wananchi wanaoishi karibu na mtambo huo na kuhatarisha afya zao:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kunusuru afya na maisha ya Wananchi wanaoishi karibu na mtambo huo.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

167. MHESHIMIWA VEDASTUS MATHAYO MANYINYI (MUSOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Serikali katika kuhakikisha inapata Watumishi bora na wenyе sifa iliamua kuwaondoa Watumishi wasio na sifa pamoja na wenyе vyeti feki, lakini zoezi hilo lilikumbwa na changamoto mbalimbali ambapo Afisa Utumishi aliwaondoa Watumishi kwenye *payroll* bila sababu maalum na walipofuutilia Wizarani walirudishwa kazini:-

- (a) Je, kwa nini Serikali isiunde timu maalum ili ipite kila Halmashauri kupitia taarifa juu ya zoezi hilo ili haki itendeke hasa kwa wale ambao hawana uwezo wa kwenda Wizarani;

- (b) Wapo Watumishi ambao baada ya kuajiriwa kwa kutumia vyeti feki walijiendeza kielimu zaidi ya Darasa la Saba na wameondolewa kwa kosa la udanganyifu wa vyeti; Je, Serikali haioni kuwa hao ni bora kuliko wale ambao hawakuijendeza.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

168. MHESHIMIWA MARYAM SALUM MSABAHA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kumekuwa na baadhi ya Askari barabarani wanaosimamisha magari hasa yale ya safari ndefu wakitokea vichakani (kujificha) na hatimaye wakati mwingine kusababisha ajali:-

Je, ni Askari wangapi kama hawa wameshachukuliwa hatua za kinidhamu.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

169. MHESHIMIWA DEOGRATIAS FRANCIS NGALAWA (LUDEWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Serikali iliahidi kulipa fidia Wananchi

walioachia maeneo yao kupisha miradi ya makaa ya mawe, Mchuchuma na Liganga lakini mpaka sasa hawajalipwa:-

- (a) Je, ni lini Serikali italipa fidia hizo ili Wananchi husika waendelee na shughuli nyingine za kiuchumi;
- (b) Je, kwa nini Serikali haitoi mrejesho pindi panapotokea mkwamo;
- (c) Je, Serikali inaweza kuthibitisha miradi hiyo itaanza kutekelezwa kama ilivyoahidi Bungeni.

170. MHESHIMIWA SILAFU JUMBE MAUFI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Mkoa wa Rukwa umeanzishwa mwaka 1974 lakini hadi sasa hakuna Viwanda vikubwa viliwyowekezwa na kuwekewa mikakati na Serikali na Viwanda viliwyopo ni vya Watu binafsi:-

- (a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kujenga Viwanda au kupeleka Wawekezaji ambao watajenga Viwanda vikubwa Mkoa wa Rukwa ili kutoa ajira kwa Vijana;

- (b) Mazao yanayolimwa Mkoa wa Rukwa yanapewa bei kiholela na kufanya maisha ya Wananchi kuwa magumu; Je, ni lini Serikali itaingia Mkataba na Viwanda vya uzalishaji.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

171. MHESHIMIWA NURU AWADH BAFADHILI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Katika kipindi cha miaka ya 1970 wakati Wanafunzi wakienda likizo Walimu nao walikuwa wakienda katika Vyuo mbalimbali vilivyokuwa jirani na Wilaya zao ili kupewa mafunzo au kupigwa msasa (*refresher course*) kiasi kwamba Walimu walikuwa wanapata ari ya kufundisha vizuri:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha utaratibu huu kwa Walimu kupigwa msasa.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

172. MHESHIMIWA JULIUS KALANGA LAIZER (MONDULI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvvi:- Tanzania ni Nchi ya 3 Afrika kwa kuwa

na idadi kubwa ya Mifugo takribani milioni 25 lakini Sekta hii bado mchango wake katika pato la Taifa ni mdogo ukilinganisha na idadi ya mifugo tuliyonayo:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Viwanda vya Nyama, Ngozi na Maziwa hapa nchini ili kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na Mifugo;
- (b) Je, ni lini Serikali itaanza kutoa ruzuku ya dawa kama Ndigana kali, Mapafu na Dripu kwa Wafugaji wetu nchini.

**173. MHESHIMIWA AUGUSTINE VUMA HOLLE
(KASULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:- Migogoro ya Wafugaji na Wakulima nchini imekuwa ya kudumu na hivyo kusababisha vifo kwa watu na uharibifu wa mali:-

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka kuja na Sera ya kupunguza idadi ya Mifugo nchini ili kuwa na ufugaji wenye tija.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

- 174. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Mgogoro wa mipaka kati ya Kijiji cha Kikulyungu na Hifadhi ya Selous ni wa muda mrefu:-

Je, Serikali itamaliza lini mgogoro huo.

WIZARA YA MAJI:

- 175. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Maji:- Miradi ya maji katika Vijiji vya Lupunga, Ruvu, Dosa na Kipandege Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha bado inasuasua mpaka sasa:-

Je, ni lini miradi hiyo itapatiwa fedha ili iweze kukamilika.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.



(Majadiliano yanaendelea)



S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE

DODOMA

06 MEI, 2019